

Wanafunzi wa Mwaka wa Mwisho katika Shule ya Lakeside High Wafika Nusu Fainali ya Mashindano ya Ufadhili wa Masomo ya National Merit Scholarship

Shirika la National Merit Scholarship Corporation lilitangaza Septemba 11 kuwa wanafunzi watatu bora wa shule ya upili katika DCSD wametajwa kufuzu kwa nusu fainali ya Mpango wa National Merit Scholarship (Mpango wa Kitaifa wa Ustahili wa Ufadhili wa Masomo) wa mwaka huu.

Wanafunzi wa mwaka wa mwisho wa Shule ya Lakeside High, Henry Fonder-Kristy, Andrew Heller na Edward Rauch ni mionganini mwa wanafunzi 16,000 waliofuzu nusu fainali kote nchini. Sasa wanashindania ufadhili wa wanafunzi 6,870 kutoka National Merit Scholarships wa jumla ya karibu dola milioni 26. Washindi wa shindano hili wanaweza kupokea hadi \$2,500 kutoka National Merit Scholarship Corporation, pamoja na kiasi ambacho hakijatajwa kutoka kwa tuzo za Merit Scholarship zinazofadhiliwa na makampuni na tuzo za Merit Scholarship zinazofadhiliwa na vyuo.

Wahitimu wa nusu fainali walichaguliwa kulingana na rekodi bora za kimasomo, mapendekezo ya shule, insha walizoandika, na alama za SAT au ACT zinazostahiki. Ili kuhitimu, wahitimu wa nusu fainali na maafisa wa shule ya upili lazima wawasilishe maombi ya kina ya ufadhili wa masomo ambayo yanajumuisha rekodi za kimasomo, ushiriki katika shughuli za shule na jamii, uwezo dhahiri wa uongozi, ajira, na heshima na tuzo.

Wahitimu wataarifiwa mnemo Februari, na wapokeaji wote wa National Merit Scholarship watachaguliwa kutoka kwa kundi hili.

Kundi la kitaifa la waliofuzu nusu fainali, ambalo linajumuisha chini ya asilimia moja ya wanafunzi wa mwaka wa mwisho katika shule za upili za Marekani, linawakilisha wanafunzi waliopata alama za juu zaidi kutoka kila jimbo. Idadi ya waliofuzu nusu fainali katika jimbo inalingana na asilimia ya jimbo ya jumla ya kitaifa ya wanafunzi wanaohitimu.

Kwa maelezo zaidi kuhusu Mpango wa National Merit Scholarship, angalia <https://www.nationalmerit.org/>.

XXX